# MWONGOZO WA MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

**(Wahariri: D.W Lutomia na Phibban Muthama)**

## JALADA

Jalada ni sehemu iliyoko juu ya kitabu hasa huwa ngumu na mambo yaliyo muhtasari wa kile msomaji anataraji ndani. Jalada huwa kuwili yaani, jalada la mbele na la nyuma. Kunavyo vipengele muhimu hasa rangi za michoro na maandishi.

Jalada lina anwani **Mapambazuko ya Machweo** na hadithi nyingine. Chini ya anwani hii kuna picha za watu watatu wazima na za watoto wawili. Picha ya mtu wa kwanza aliyevalia suti ya kijani kibichi, tai na miwani na kuonekana kuingia gari jekundu inasawiri tajiri aliyekuja kumtuza mzee Makucha.

Picha ya pili ya mwanaume anayeonekana kufurahi na pesa mkononi inamsawiri mhusika mzee Makucha ambaye amefurahia kupokea tuzo baada ya kuwaokoa watoto wadogo waliokuwa wakifanya kazi migodini mwa mzee Makutwa.

Picha ya tatu ya mwanamke anayefurahi pamoja na mwanaume wa pili inamsawiri Bi. Macheo, mkewe mzee Makucha, anayejiunga naye kufurahia tuzo aliyopewa mumewe. Nyuma yao kuna nyumba ambayo ina mabati yaliyozeeka inayoashiria hali ngumu ya kiuchumi ambayo familia ya mzee Makucha imepitia baada ya kufutwa kazi na Shirika la Reli.

Aidha, kuna picha ya watoto wawili: msichana na mvulana wanaofanya kazi ngumu. Msichana amebeba besini na mvulana ameinama kupakuwa mchanga kwenye kijiko. Wanaonekana wamechafuka. Picha hii inarejelea watoto wanaofanya kazi ngumu katika mgodi wa mzee Makutwa wanaookolewa baadaye na mzee Makucha.

Chini ya jalada upande wa kulia kuna meza na kiti. Juu ya meza kuna bidhaa mbalimbali za kuuzwa kuonyesha biashara iliyokuwa ikifanywa na familia ya mzee Makucha.

Pia kuna mwanga wa jua unaowamulika mzee Makucha, Bi. Mchewa na wale watoto wawili. Mwangaza huu **ni ishara ya matumaini** au **fikra endelevu katika jamii**. Unaweza kurejelea kitendo cha mzee Makucha kuwaokoa watoto waliokuwa wakifanya kazi migodini au tuzo anayopata mzee Makucha kwa kitendo hicho cha kuwaokoa watoto.

## 1. FADHILA ZA PUNDA - (Rachel Wangari)

### MUHTASARI

- Lilia ni msichana mcha Mungu. Amelelewa katika mandhari ya dini na babake, pastor Lee Imani, ambaye ndiye mhubiri mkuu kanisani mwao. Mamake Lilia ameshafariki katika ajali ya barabarani.
- Kanisani, anajitokeza Luka ambaye ni mvulana maskini ila ana sauti nzuri ya kuimba, kitu ambacho kinamvutia sana Lilia. Lilia anamrai babake kumsaidia Luka. Luka anapelekwa shuleni na mamake anapewa kibarua cha kunadhifisha mazingira kanisani kwa babake Lilia.
- Miaka inavyosonga ndivyo babake Lilia anaingiwa na hofu kuhusu mahusiano kati ya bintiye na Luka. Hivyo, anamtuma Luka kusomea sehemu nyingine ya nchi huku akiishi kwa mhubiri mwenzake. Badala ya urafiki kufifia, unageuka na kuwa mapenzi. Baadaye,

Luka na Lilia wanaishia kusoma katika Chuo kimoja na hatimaye Lilia anamrai babake amruhusu kupendana na Luka.

- Baada ya masomo yao, Luka anapewa majukumu ya uhubiri kanisani na ruhusa ya kumuoa bintiye mhubiri mkuu. Wanafunga ndoa na Luka anakuwa maarufu katika kazi yake kanisani mpaka watu kutoka nchi mbalimbali wanakuja kanisani humo kwa ajili ya miujiza aliyoifanya.
- Baada ya babake Lilia kufariki, Luka anatwaa uongozi wa kanisa kwa muda kabla ya kumwachisha mkewe kazi katika benki ili kuwa karibu zaidi kwa utumishi wa kanisa. Ndoa yao inaanza kuwa na matatizo
- Luka anapoamua kuacha kazi ya uhubiri na kuwa mwanasiasa. Wakati huu, mkewe ashakuwa mke wa nyumbani, anatawishwa. Luka, ambaye alikuwa mhubiri wa injiii, anageuka kuwa mwanasiasa na mume katili kwa mkewe, mkombozi wake wa utotoni. Ukatili wake unadhihirika tangu mwanzo mpaka kufikia wakati anamuumiza sona. Lilia anachukuliwa na mama mkwe wake, Luka, na kupelekwa hospitatini kupata matibabu kwa maumivu anayopata kutokana na kichapo cha mumewe. Wakati huo huo, Luka anapata ajali mbaya ya barabarani na kuumia sana. Anatozwa katika chumba kimoja na mkewe. Baadaye, kwamba Luka huenda asiweze kutembea tena kutokana na athari za ajali. Kimada wake anapopata taarifa hii, anapotea kabisa asirudi hospitalini kumjulia hali. Inakuwa kwamba kwa kumtetekeza mkewe, Luka anaacha mbachawe kwa msala upitao,

**Mandhari ya hadithi**

Mandhari ya hadithi hii ni mashamboni na pia mjini. Lilia anakutana na Luka mora ya kwanza mashambani anapokuja kanisani. Wanaendelea kuishi huko. wakati mmoja Luko akienda kusomeo katika sehemu tofauti yo nchi. Hata hivyo, Luka anapokuwo Gavana anaishi mbali na nyumbani, mjini.

**UFAAFU WA ANWANI**

- Luka analiuza kanisa ambalo limemfaa muda mrefu na kumpa umaarufu nchini.
- Baada ya Luka kumrai Lilia kuacha kazi anakuja kumdharau na hata kumdhihaki kuwa kazi yake ni kula na kulala tu.
- Baada ya Luka kuchaguliwa gavana anasahau na kukosa kutimiza ahadi zote za kisiasa alizowaahidi.
- Baada ya Senior Pastor Lee Imani, babake Lilia, kumkubalia Luka kumwoa Lilia,Luka alipuuza baraka alizopewa na babake Lilia akamtesa mkewe.
- Luka hahuzuniki Lilia anapopoteza ujauzito uliotoka kutokana na Lilia kukesha usiku kucha akisubiri mumewe ambaye hakurudi nyumbani usiku huo.
- Baada ya Lilia kumpenda Luka hata akamrai babake kukubali uchumba "'.vao, Luka analipa kwa uzinzi na mapigo.
- Lilia anapomtembelea mumewe ofisini kumwona katikati ya juma na kusubiri hadi arudi, mumewe anaporudi na kumpata mapokezini anamfokea na kumwelekeza arudi nyumbani.
- Baada ya Lilia kuandamana na mumewe kwenye hafla ya kisiasa anapotafuta kura, akishakuwa Gavana anamshauri arejee kuishi kijijini ambapo kwa nadra angemwona mwishoni mwa wiki.

- Jioni Luka aliporejea nyumbani Lilia alienda kumfungulia mlango kwa hamu kuu ila badala ya salamu na dundu la mumewe, alipokezwa kofi na teke.
- Luka anamtawisha Lilia nyumbani na kumpigia marufuku ya kutoka nyumbani. Hii ni kwa sababu aliogopa Lilia angetoka nje ingemwanika mbcle ya wapinzani wake. Awali Luka alipenda kutembea na mkewe ili aonekane kama mwanafalüilia bora.
- Hawara wa Luka aliyeaminiwa kuwa mshauri wake, anamtoroka baada ya ajali licha ya kuwa naye kila wakati na kujistarehesha kila wakati
- Badala ya Lilia kurithi mali/biashara ya babake (kanisa), ni mumewe ndiye anayelirithi. Kanisa hili lilianzishwa na babake Lilia.
- Ni jukumu la wanawake kunyamazia maovu kwenye ndoa ili kudumisha amani kwenye ndoa zao.(uk 5)
- Wanawake wanatumiwa na waume zao ili kusawiri hadhi bora kifamilia. Luka anamwandama Lilia ubavuni mwake kama taswira ya kiongozi anayethamini ndoa na familia yake. Lengo lake ni kuchaguliwa na raia.(uk 5)
- Lilia angekataa kuandamana na mumewe anatusiwa kuwa mnene kama nguruwe na kuwa hana kazi maalumu.(uk 5)
- Wanawake kama Lilia wakikataa kutekeleza haja za waume zao hutishiwa. Lilia anatishiwa kuwa wanawake ni wengi.(uk 5)
- Wanawake wanatumiwa kama vyombo vya starehe. Luka ana hawara tele licha ya kuwa na mke.(UK 5)
- Wanawake huwangoja '.vaurne zao kurejea nyumbani kabla hawajalala.Lilia anamgojea Lukausiku kucha hadi anapoteza ujauzito.(UK 5)
- Luka anamtenga Lilia kuishi kijijini ili kuwahakikishia raia wapiga kura kuwa Gavana yu karibu.(UK 5)
- Wanawake wanahita)i miadi kabla hawajawatembelea waume zao. Luka anamfahamisha Lilia kuwasiliana na mhazili wake akapewe miadi ndiposa amtembelee.(uk 6)
- Wanawake wananyimwa nafasi ya kutoka nyumbani. Luka anamtisha Lilia kuwa akitoka nje ya lango atajua kilichomtoa kanga manyoya shingoni. Wanawake wanatengwa na marafiki zao. Lilia amejitenga na marafiki take maanake kila wakimtembelea mumewe anajua na kuishia kumpa kichapo.(uk 6)

**MAUDHUI**

**TAASUBI YA KIUME**

- Luka anampiga mkewe Lilia kwa ngumi, teke, kofi na hata kumfokea. Mara ya mwisho ilikuwa teke lililompata tumboni sawasawa, asiweze kujinyoosha kwa siku mbili kwa sababu ya maumivu makali.(uk l)
- Luka anampiga mkewe Lilia kwa kisingizio kuwa chakula hakikukolea chumvi. Uso wa Lilia umejaa kovu badala ya ngozi nyororo, vidu na tabasamu ya daima kutokana na vipigo vya mumewe.(uk l)
- Baada ya kuanza uzinzi na hawara zake, Luka anakuwa mkali kwa mkewe. Kucheka kwake kunakuwa nadra kama mwezi kupatwa; anageuka kuwa mzigo moto - habebeki kamwe.(uk l)
- Baada ya kifo cha babake Lilia, mumewe Luka anamshinikiza kuacha kazi kwa madai kuwa anamhitaji kudhibiti fedha za kanisa. (uk 4)

- Baada ya kuacha kazi Lilia anasukumiwa kazi za utawa-kukaa nyumbani kupokea utiriri wa wageni wa kanisa(wageni wa mumewe)(uk 4)
- Kazi za Lilia zinakuwa kuonekana ila si kunena.Wake hawana usemi nyumbani.(uk 5)
- Ushauri wa wanawake unapuuzwa. Lilia anambembeleza mumewe asiingilie siasa ila Luka alishatunga na akishatunga habadili.(uk 5)
- Luka analiuza kanisa lao pasi na kummshauri wala kumwuliza mkewe Lilia. Lilia anatanabahi kanisa limeuzwa.(uk 5)
- Badala ya Lilia kurithi mali/biashara ya babake (kanisa), ni mumewe ndiye anayelirithi. Kanisa hili lilianzishwa na babake Lilia.
- Ni jukumu la wanawake kunyamazia maovu kwenye ndoa ili kudumisha amani kwenye ndoa zao.(uk 5)
- Wanawake wanatumiwa na waume zao ili kusawiri hadhi bora kifamilia. Luka anamwandama Lilia ubavuni mwake kama taswira ya kiongozi anayethamini ndoa na familia yake. Lengo lake ni kuchaguliwa na raia.(uk 5)
- Lilia angekataa kuandamana na mumewe anatusiwa kuwa mnene kama nguruwe na kuwa hana kazi maalumu.(uk 5)
- Wanawake kama Lilia wakikataa kutekeleza haja za waume zao hutishiwa. Lilia anatishiwa kuwa wanawake ni wengi.(uk 5)
- Wanawake wanatumiwa kama vyombo vya starehe. Luka ana hawara tele licha ya kuwa na mke.(UK 5)
- Wanawake huwangoja '.vaurne zao kurejea nyumbani kabla hawajalala.Lilia anamgojea Luka usiku kucha hadi anapoteza ujauzito.(UK 5)
- Luka anamtenga Lilia kuishi kijijini ili kuwahakikishia raia wapiga kura kuwa Gavana yu karibu.(UK 5)
- Wanawake wanahita)i miadi kabla hawajawatembelea waume zao. Luka anamfahamisha Lilia kuwasiliana na mhazili wake akapewe miadi ndiposa amtembelee.(uk 6)
- Wanawake wananyimwa nafasi ya kutoka nyumbani. Luka anamtisha Lilia kuwa akitoka nje ya lango atajua kilichomtoa kanga manyoya shingoni. Wanawake wanatengwa na marafiki zao. Lilia amejitenga na marafiki take maanake kila wakimtembelea mumewe anajua na kuishia kumpa kichapo.(uk 6)
- Nanawake hawafai kuwashtaki waume zao. Lilia anapothubutu kusema angemshtaki mumcwe inakuwa kama kuchokoza nyuki, anapigwa.(uk 6)
- Wanawake hawafai kuulizia hawara za waume zao. Lilia anapouliza mwanamke aliyemwona ameandamana na mumewe kwenye vyombo vya habari, alijibiwa kwa kipigo kilichomlaza kitandani siku mbili.(uk 7)
- Lilia anapigwa kipigo cha kifo kwa kujaribu kuripoti mumewe kwenye kituo cha polisi. Japo hakumripoti, kuonekana kwenye kituo cha polisi ndicho kinachomletea vipigo.(uk 7)

**DINI**

ILI KUPATA MWONGOZO NZIMA PIGA SIMU KWA 0724351706

MWONGOZO NZIMA INA KURASA 110

## PIA KUNA

1. MWONGOZO WA NGUU ZA JADI
2. MWONGOZO WA KIGOGO
3. MWONGOZO WA TUMBO LISILOSHIBA
4. MWONGOZO WA CHOZI LA HERI
5. MASWALI NA MAJIBU YA MAPAMBAZUKO
6. MTIHANI WA SHULE ZA KITAIFA MBALIMBALI
7. MITIHANI YA KATI YA MUHULA
8. MITIHANI YA MWISHO WA MUHULA
9. TINI YA ISIMUJAMII, FASIHI SIMULIZI, SARUFI NA USHAIRI
10. MASWALI NA MAJIBU YA CHOZI, KIGOGO NA TUMBO

**TUNA MENGI- PIGA SIMU KWA 0724351706**